Busara ni mwanafunzi wa Darasa la Saba katika Shule ya Msingi Tumaini. Anaishi na bibi yake katika Kijiji cha Mwendokasi. Kijiji hicho kipo karibu na Hifadhi ya Wanyama ya Mkomazi. Siku moja Jumamosi, Busara na bibi yake walijihimu kuelekea shambani.Wakiwa wanakaribia kufika shambani, Busara aliwaona wanyama wawili kwa mbali wakitembea kuelekea upande walikokuwa wakielekea wao. Alimshika bibi yake mkono kwa woga, huku akisema, "Bibi! Bibi! Unawaona wale ng'ombe?" Bibi alinyanyua shingo ili awatazame vizuri. Alimjibu huku akiwa amepigwa na butwaa kuwa wale si ng'ombe bali ni tembo. Alimuuliza tena, "Umejuaje kuwa ni tembo?" Bibi alimjibu, "Nawaona kwa mbali ni wanyama wakubwa kuliko ng'ombe. Wana masikio makubwa na mikonga imetangulia mbele." Waliamua kusimama ili waangalie wanakoelekea. Mara, waliwaona tembo wakiingia kwenye shamba la mahindi na alizeti.